

Mabasi 49 mapya ya kisasa mwendokasi yawasili

Na Lidya Inda

MABASI mapya na ya kisasa 49 ya Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) yamewasili nchini yakiwa ya hadhi ya kimataifa.

Mabasi hayo ya Golden Dragon yaliyotengenezwa China, ni sehemu ya mabasi 99 ya mpango wa Serikali ya Awamu ya Sita kuleta mageuzi ya usafiri wa mijini.

Tofauti na mabasi ya awali, yaliyowasili sasa yana mfumo wa kisasa wa viyoyozi na vitundu vya kuchajia simu katika kila kiti, teknolojia ambayo awali ilizoeleka kuonekana kwenye treni la Reli ya Kisasa (SGR),

mabasi ya kisasa na kwenye ndege.

"Sasa, abiria wa Kimara, Korogwe, Mbezi, Morocco watasafiri kwa hadhi ya kimataifa huku mawasiliano yao yakibaki hewani wakati wote. Tunampa kongole ya dhati Rais Samia Suluhu Hassan," ilieleza taarifa iliyotolewa na Kampuni ya Mabasi Yaendayo Haraka (UDART).

Mafanikio hayo yametajwa kuwa matunda ya ushirikiano kati ya viongozi wabunifu wa Udart na Wakala ya Mabasi Yaendayo Haraka (DART) wanaotafsiri maono ya Rais Samia.

Akipokea mabasi hayo bandarini jana, Pius

Ng'ingo alisema, "Dhamira ya Rais ni kumpatia mkazi wa Dar es Salaam huduma bora anayostahili. Mabasi haya 49 ni mwanzo tu, mengine 50 yanakuja hivi karibuni. Tuko katika hatua za mwisho za usajili na ukaguzi ili yaingie barabarani haraka iwezekanavyo."

Aidha, taarifa hiyo iliongeza kuwa Mradi wa BRT Dar es Salaam umekuwa maabara ya mafunzo kwa mataifa mengi ambao mataifa kama Singapore, Algeria, Ufilipino, Afrika Kusini, Kenya, Uganda, Ethiopia, Rwanda na Nigeria yamekuwa yakituma wataalamu wao Dar es Salaam kujifunza mfumo wa usimamizi na miundombinu.

"Hata nchi za mbali kama Vietnam na baadhi ya miji ya India zimevutiwa na jinsi Tanzania ilivyoweza kusanifu mradi huu katikati ya changamoto za ukuaji wa kasi wa miji," iliongeza taarifa ya Udart.

Mwanzoni mwa wiki, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Profesa Riziki Shemdoe alithibitisha kuwa serikali imetenga Sh bilioni 20 kwa ajili ya ununuzi wa mabasi yote 99.

Alisisitiza kuwa uwekezaji huo ni endelevu na unalenga kuhakikisha usafiri wa umma unakuwa salama, wa bei nafuu na wa uhakika.

Daily News Saturday January 10, 2026 Pg 2

State to consider stakeholders views on fatigue rules

By **SAMWEL MWALONGO**

THE government has assured transport stakeholders that it will take into account their views on the draft 2026 Land Transport Regulatory Authority (LATRA) regulations on the management of driver fatigue.

During consultations, stakeholders raised concerns over the proposed maximum driving time for passenger vehicle drivers. The draft regulations recommend that a driver

should not drive for more than nine hours within a 24-hour period.

However, stakeholders suggested that the rules should instead consider the distance travelled, citing challenges such as traffic congestion, particularly for vehicles operating between Dar es Salaam and up-country regions.

Another concern highlighted was the offences and penalties for non-compliance. According to the draft regulations, a vehicle owner who violates the rules would face a

fine ranging from 200,000/- to 500,000/-, while drivers will be fined between 100,000/- and 200,000/-.

Speaking at the closing of a stakeholders' consultative meeting on the draft regulations held in Dar es Salaam on Thursday, LATRA Assistant Director for Road Transport Services in the Ministry of Transport, Mr Andrew Magombana, said the process is still ongoing and open to further input.

"This process has not yet reached the final stage. The Authority's objective is to ob-

tain constructive views that will help in making the right decisions in the national interest," he said.

Mr Magombana urged stakeholders to continue submitting their recommendations in writing within 14 days from Thursday, to ensure all parties have an opportunity to participate fully.

Earlier, LATRA Director, CPA Habibu Suluo, explained that driver fatigue remains a major challenge with serious implications for passenger safety, investors' interests and the

national economy.

He noted that road accidents continue to be reported, many linked to driver fatigue, with some causing significant losses to investors and the country.

Mr Suluo stressed that the regulations are not intended to oppress investors but to protect their interests, safeguard drivers' health and ensure passenger safety.

"When an accident occurs, you lose passengers' lives, property, and the vehicle itself is damaged," he said.